BMS

# MTIHANI WA KISWAHILI
# DAR. LA 8 MUHULA WA II-2020

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali **50.**
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**JINA LAKO**

**JINA LA SHULE YAKO** **Muda: Saa 1 dakika 40**

**Chagua jibu lifaalo kujazia nafasi 1-15.**

Usiku ni __1__ mrefu na mwafaka wa __2__ kufanywa kote duniani. Labda ni uwepo wa __3__ cheusi au kwa vile watu wengi hupatikana __4__ pao nyakati hizi. Hizi zote hazifai kuwa sababu. __5__ haya, huu ndio wakati __6__ wa kupumzika na kujumuika na jamaa baada ya gange za __7__. Giza __8__ limewafanya watu kuvumbua mwangaza wao na __9__ kila pahali ili __10__ wenye njama kama hizo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. masaa | B. mda | C. wasaa | D. nyakati |
| **2.** | A. mathila | B. mageni | C. maovu | D. mema |
| **3.** | A. giza | B. usiku | C. mwangaza | D. kiza |
| **4.** | A. mastakimu | B. mastakimuni | C. makazi | D. makao |
| **5.** | A. Kando na | B. Kinyume cha | C. Kinyume na | D. Fauka ya |
| **6.** | A. mzuri | B. nzuri | C. finyu | D. mbovu |
| **7.** | A. kutwa | B. kucha | C. juma | D. ngarange |
| **8.** | A. hii | B. yenyewe | C. hili | D. huu |
| **9.** | A. kutanda | B. kutandua | C. kuanika | D. kutundika |
| **10.** | A. kuwaongopa | B. kuwaogopea | C. kuwahofia | D. kuwaogofya |

Masoko makubwamakubwa yana __11__ ya kupatwa na __12__ ya moto usiojulikana wazi vianzo __13__. Ni visa vya __14__ sana kwani husababisha hasara kubwa __15__. Mfano bora na hai ni soko la Gikomba jijini Nairobi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. mazoea | B. uzoefu | C. tabia | D. umaarufu |
| **12.** | A. mikasa | B. visa | C. mikosi | D. vikosi |
| **13.** | A. vyenyewe | B. vyote | C. yao | D. vyao |
| **14.** | A. kuajabia | B. kusikitisha | C. kutingisha | D. kuhofisha |
| **15.** | A. zinazokadiriwa | B. inayokadiriwa | C. zisizokadirika | D. visivyokadirika |

**Jibu maswali kutoka 16-30 kwa kufuata maagizo uliyopewa:**

**16.** Chagua sentensi iliyotumia Kiunganishi sahihi.
A. Wanafunzi wa shule hii huja angalau kila asubuhi.
B. Wagonjwa wale walikimbizwa hospitalini maadamu wapone.
C. Mwalimu hajaja darasani, aidha hakutuwachia kazi ya ziada.
D. Mlinzi anazo pesa madhali hajalipwa mshahara.

**17.** Gwiji wa kuyaimba mashairi kwa maghani tofautitofauti ni
A. mghani B. mandhuna
C. sogora D. manju

**18.** Kuuma huu na hasara juu kuna maana ipi?
A. Kuumia sana
B. Kupoteza kila kitu
C. Kuibiwa
D. Kutokuwa na bahati katika kila jambo

**'Ki' kimetumikaje katika sentensi?**

**19.** Chuma kiwahi kingali moto.
A. Ki - udogo
B. Ki - masharti
C. Ki - ngeli
D. Ki - kutofanyika

**20.** Toa maelezo sahihi ya 'kukanza' kama inavyotumiwa katika upishi.
A. Kukipasha chakula joto baada ya kupoa.
B. Kukipoza chakula.
C. Kutia viungo mbalimbali kwenye chakula.
D. Kupika chakula kwa mafuta pekee.

**21.** Mshororo wa tatu katika shairi huitwaje?
A. Mleo
B. Mloto
C. Utatu
D. Tathlitha

**22.** Andika kinyume cha maneno haya: **Choma na meza.**
A. Chomeka na kunywa
B. Chomoza na tema
C. Chomoa na toa
D. Chomoa na tema

**23.** Ni sentensi ipi imeandikwa kwa hali ya Kutendesha vizuri.
A. Mtoto ameamshwa na kelele.
B. Utingo alimshukisha abiria pasipofaa.
C. Ng'ombe amelemewa sana na ugonjwa.
D. Dereva alisimamishwa ili kushusha abiria mlevi.

**24.** Mtu aliyepinduka vidole kwa ndani huitwaje?
A. Kibyongo B. Kiduko
C. Kikono D. Kibwiko

**25.** Ni maelezo yapi si sahihi kuhusu **Panda**?
A. Aina ya mnyama
B. Aina ya silaha
C. Bei kudidimia
D. Kwea kama vile mti


**26.** Kauli ipi sahihi?
A. Matopa ya vitabu
B. Vururu ya matope
C. Umati wa vifaranga
D. Finyu la mboga

**Andika wingi wa sentensi hii:**

**27.** Taa ya gari ilimchanganya nyani.
A. Mataa ya magari yaliwachanganya manyani.
B. Taa za magari ziliwachanganya manyani.
C. Mataa ya magari ziliwachanganya nyani.
D. Taa za magari ziliwachanganya nyani.

**28.** Watoto wa ngurue wanaitwaje?
A. Vicheche B. Vivinimbi
C. Vinyemere D. Viyoyo

**29.**



Umbo lililochorwa hapo kando linaitwaje?
A. Hiram
B. Dandalo
C. Msalaba
D. Ngoe

**30.** Salamu ipi kati ya zifuatazo hutumika asubuhi tu?
A. Chewa
B. Masalkheri
C. Buriani
D. Je, wambaje?

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.**

Katika dunia hii, kila mtu yu mbioni kutafuta mali ili kuboresha maisha. Ukiwa na pesa nyingi utaweza kuwa na nyumba nzuri, chakula bora na mavazi aula. Ukiugua, bila shaka utapata matibabu bora na hivyo kuwa na tumaini la kula chumvi nyingi.

Kuna baadhi ya vitu ambavyo huwezi kuvipata kwa sababu una mali mengi. Ustaarabu, hekima na afya bora ni majaliwa kutoka kwa Muumba. Hospitali za kifahari zimejaa wakwasi ambao kando na

uchungu wa kuugua, wanahofia kuacha mali yao. Ugonjwa pamoja na woga hatima yake ni mauko.

Ukwasi unaoleta furaha ni ule ambao umepatikana kwa kutoa jasho. Ukiwa mchumia juani basi unapolia kivulini utakuwa umetulia na kuterema. Usiku utalala usingizi wa pono bila jinamizi. Kwa upande mwingine, ukwasi uliotafutwa kwa njia za hila hauleti furaha. Mchana kutwa na usiku kucha ni taabu. Huogopa pengine aliowatapeli mali yao huenda wakapanga njama ya kumwangamiza. Usingizi kuupata ni shida na aupatapo hukaribishwa jinamizi.

Kwa upande mwingine, mtu mwenye mapato ya chini hutaabika mchana akajitafutia akiwa na matumaini kuwa ipo siku ambayo atafanikiwa. Afikapo nyumbani usiku, usingizi humlemea na kulala fofofo. Njozi zake huwa za matumaini. Anaweza kuota akiwa mfalme, mkwasi au kwenye sherehe akigwegwenya minofu ya nyama au ameandaliwa chakula kilichojaa chinyango. Tatizo ni kuwa ruya haiwezi kukuruhusu kula. Unapojianda kukipeleka chakula mdomoni, umeamka. Ukilala tena, ndoto haijiendelezi, pengine ianze nyingine.

Nikichunguza kwa makini, ninaamini kuwa ndoto ni jumla ya mawazo ambayo umekuwa ukiyafikiria mchana. Ninapozungumza kuhusu ukwasi na ufukara, simaanishi kuwa ninapendelea ufukara. La hasha. Ningependa watu watafute mali kwa njia inayofaa. Hakuna fahari ya kuwa na ngwenje chafu. Uchafu wake utasumbua hata dhamira yake. Tutajivunia taifa likiwa na watu safi wenye mali safi. Usafi wa mwili, usafi wa mawazo na usafi wa mapato utaliongoza taifa kuwa salama pasi na hofu yoyote ya majambazi; wezi au wahuni.

**31.** Ni kipi ambacho pesa nyingi haziwezi kukuletea?
A. Maisha marefu
B. Makazi mazuri
C. Mavazi mazuri
D. Utapiamlo kwa wana wake

**32.** Kwa nini kila mtu yu mbioni kutafuta mali?
A. Kupata vyakula bora na kuwadunisha wengine.
B. Kuishi maisha bora na kuwa na afya nzuri.
C. Kupata matibabu bora na hatimaye mauko.
D. Kupata chakula bora, mavazi uchwara na matibabu bora.

**33.** Mkwasi anaweza kufa haraka iwapo
A. hana chakula bora na nyumba duni.
B. anahofia kuiacha mali yake anapougua.
C. anapata matibabu bora katika hospitali ya kifahari.
D. hana pesa za matumizi.

**34.** Ni bwenyenye yupi ambaye kwa kawaida hana furaha?
A. Yule ambaye ni maskini hohehahe.
B. Aliyetajirika kwa njia isiyofaa.
C. Aliyeshindwa na wenzake kwa ukwasi.
D. Mwenye afya nzuri kutokana na matibabu bora.

**35.** Mwandishi ana mawazo gani kuhusu ndoto?
A. Ndoto huwa kinyume cha fikira za binadamu.
B. Ukiota ndoto ni lazima mambo hayo yatokee.
C. Kila mtu ni lazima aote.
D. Ndoto huwa ni mambo yaliyokuwa kwenye fikira.

**36.** Ni nani ambaye hawezi kupata usingizi wa pono?
A. Maskini B. Tapeli
C. Tajiri D. Mtoto

**37.** Kwa nini fukara anaweza kuota akigwenyagwenya minofu au akiwa ameandaliwa chakula kilichojaa minofu?
A. Mawazo yake yalikuwa yakimwelekeza kuwa kuna siku atafanikiwa na kuishi vizuri.
B. Alikuwa akila minofu mchana kutwa kwa hivyo ni marudio.
C. Kila mtu anapenda chinyango na watu wengi huota hivyo.
D. Walikuwa wamehudhuria sherehe iliyokuwa na mapochopocho kwa wingi.

**38.** Kulingana na maoni ya mwandishi
A. ndoto haikamiliki
B. ndoto hukamilika
C. ndoto zote ni za kutisha
D. maskini huwa na jinamizi kuliko tajiri

**39.** Kuna maana gani unaposema kuwa kuna pesa chafu?
A. Kuna pesa zilizochakaa kwa kutumika kwa muda mrefu.
B. Mtu asiyezingatia usafi wa mwili, pesa zake ni chafu aidha.
C. Pesa ambazo zimepatikana kwa njia isiyofaa zinasemekana kuwa chafu.
D. Pesa ni chafu kwa sababu zimepitia kwa watu wengi.

**40.** Mwandishi ametaja usafi wa aina ngapi?
A. 2 B. 4
C. 3 D. 5

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.**

Fatuma alikiona kilichomfanya kuku kukosa meno hivi hivi juzi juzi. Huku michirizi ya machozi ikimchirizika, na akiwa na uchungu mwingi alisikika akilia kwa kusema, "Ole wangu. Majuto ni mjukuu, kama ningalijua nisingalitoa mimba hivyo. Sasa nimebaki na kaburi mwilini. Mungu, naomba unisamehe kwa kuua kiumbe chako bila sababu yoyote.

Fatuma, msichana wa miaka kumi na minane alipata mimba hiyo akiwa kidato cha nne. Alienda kwa mganga wa kichochoroni na mganga huyo alipokuwa akitoa mimba hiyo, Fatuma alianza kuvuja damu nyingi hadi akazirai. Mganga kuona mambo yalivyokuwa yakizidi kuwa mabaya alimuacha hapo kitandani na kutimua mbio. Kwa bahati nzuri msamaria mwema alimchukua msichana huyo hadi kituo cha matibabu alikolazwa huko kwa muda wa miezi mitatu.

Jambo la kuhuzunisha na lililomtia Fatuma hofu sana ni kujua kuwa alikuwa ameyaangamiza maisha ya kiumbe cha Mungu. Mawazo hayo yangali yanamtatiza mpaka leo na kila anapokumbuka kitendo hicho machozi humtoka. Isitoshe daktari pia alimfahamisha kuwa katika maisha yake yote ya baadaye, hataweza kuzaa tena kwa sababu sehemu zake za uzazi hasa nyumba ya mtoto ilikuwa imeharibika kabisa.

Uharibifu huo ulikuwa umesababishwa na vifaa ambavyo mganga huyo bandia alikuwa akivitumia kwa utoaji mimba.

---

**41.** Nini maana ya **<u>michirizi ya machozi</u>**?
A. Machozi yalimlengalenga machoni.
B. Machozi yalimjaa machoni.
C. Kulia bila kutoa sauti ya kwikwikwi.
D. Njia nyembamba ya machozi.

**42.** Maana ya Methali 'Majuto ni mjukuu' ni
A. Majuto ni mtoto wa mwanawe babu.
B. Utajuta ukimchokoza mwenzako.
C. Ukifanya matendo mabaya au kukosa utajuta baadaye.
D. Ukienda kwa mwendo wa kufanya jambo kwa wakati wake, utasikitika polepole ukijuta.

**43.** Fatuma alijiunga na shule ya upili akiwa na umri wa
A. miaka kumi na mitano
B. miaka kumi na minane
C. miaka kumi na sita
D. miaka kumi na minne

**44.** Kulingana na habari hii, baada ya kutoa mimba Fatuma alithibitishwa kuwa
A. muuaji
B. tasa
C. mganga
D. kahaba

**45.** Kwa nini mganga alitimua mbio? Kwa sababu
A. Fatuma alikuwa amefariki.
B. aliogopa damu kuvuja.
C. alikuwa ameangamiza kiumbe cha Mungu.
D. alikuwa na hofu Fatuma alipotokwa na damu nyingi kisha akazirai.

**46.** Mawazo gani yangali yanamtatiza Fatuma mpaka leo?
A. Kuangamiza kiumbe cha Mungu.
B. Fikira kuwa hatazaa tena.
C. Kuharibiwa maisha na mpenziwe Hamisi.
D. Kutokwa damu nyingi.

**47.** Ni Msemo upi ufaao kutumiwa badala ya 'Kutimua mbio'?
A. Kuenda kukuru kakara.
B. Kutimua timu timu.
C. Kwenda shoti.
D. Kwenda pukutu! Pu

**48.** Maana ya neno kuzirai ni
A. kufariki
B. kushikwa na kisunzi
C. kupotewa na ufahamu
D. kulala

**49.** Neno jingine sawa na 'Kutoa mimba' ni
A. kuavya
B. tasa
C. kuua
D. kunyonga

**50.** Nyumba ya mtoto ni
A. nyumba anamolala mtoto
B. chupa
C. mahali ambapo mtoto hupitia anapozaliwa
D. mahali mtoto anaishi akishazaliwa